**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

---

# MAELEZO YA KUJIUNGA NA CHUO CHA WILAYA CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUNYA (CHUNYA DVTC) KWA MWAKA 2025

## UTANGULIZI

Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na chuo cha VETA Chunya!

Chuo cha Wilaya cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Chunya (Chunya DVTC) ni chuo cha serikali kinachomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, yaani VETA. Chuo kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Kata ya Mbugani, karibu na Mizani; umbali wa Kilomita 1, kutoka Barabara Kuu ya Mbeya-Chunya-Makongolosi; na umbali wa kilomita 10 kufika Chunya mjini unapotokea Mbeya.

**Tafadhali, yeyote unayehusika, yaani Mwanafunzi, Mzazi au Mlezi soma kwa umakini maelezo haya ili kutekeleza mahitaji mbalimbali kuhusiana na kujiunga na chuo cha Chunya DVTC kwa Mwaka 2025.**

## MAELEZO

1. Katika kipindi hiki cha Semista ya Kwanza (Januari – Juni 2025), **kutokana na sababu za msingi**, **wanafunzi wote wamechaguliwa kwa nafasi ya Kutwa au "Day". Hata hivyo, kwa kuzingatia umbali wa baadhi ya wanafunzi, kutoka katika mikoa mingine, na hata wa ndani ya Chunya kuhitaji kufanya mafunzo wakiwa wanaishi chuoni, Chuo kimeweka utaratibu na gharama za huduma za hosteli, ambapo chakula mwanafunzi atajitegemea.**

2. Wanachuo wote wanasisitizwa kuzingatia kufika Chuoni, siku ya kufungua chuo kama ilivyoelezwa katika Barua ya Kujiunga na chuo, yaani tarehe **13 Januari 2025**. Usiporipoti ndani ya siku 14, toka tarehe ya ufunguzi, itahesabika hutaweza kufika chuoni, na nafasi uliyopewa, atapewa mtu mwingine.

3. **Tafadhali: ufikapo chuoni, fika na cheti halisi pamoja na kivuli cha cheti au taarifa rasmi ya Mkuu wa Shule uliyohitimu.**

4. Jedwali hapa chini ni mchanganuo wa ada, michango na mahitaji mbalimbali ya mwanachuo: -

| Na | MAELEZO | Semista ya 1 (Mac – Juni) | Semista ya 2 (Jul-Dis) |
|---|---|---|---|
| **a) Ada na michango** | | | |
| 1 | Ada | 30,000 | 30,000 |
| 2 | Mahafali | | |
| 3 | Serikali ya wanafunzi | 5,000 | |
| 4 | Michezo | 20,000 | |
| 5 | Ada ya mtihani | | |
| 6 | Uchakavu | 10,000 | |
| 7 | Godoro | 20,000 | 20,000 |
| **Jumla ya ada na michango** | | **85,000** | **50,000** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **(b) Sare ya Chuo** | | | |
| 1 | Suruali mbili | Atajishonea | |
| 2 | Overall/overcoat" moja | Atajishonea | |
| 3 | Fulana (T-shirt) ya VETA | Ataelekezwa rangi na maandishi | |
| 4 | Nembo mbili za VETA | Ataaweka mwenyewe | |
| 5 | Kitambulisho | 6,000 | |
| **Jumla ya gharama za sare za chuo** | | | |
| **Bima ya afya (kwa ambao hawana)** | | **NHIF** | **NHIF** |
| **Jumla (a+b+c)** | | **6,000** | |

5. Utaratibu wa kulipa ada na gharama za mahitaji mengine utakuwa kama ifuatavyo: -

| **Semista ya 1** | **Semista ya 2** |
|---|---|
| **91,000/=** | **50,000/=** |

6. Utaratibu wa kulipia ada pamoja na hela ya mahitaji mengine utafanyika kwa "**Control Number"** maalumu utakazopewa na Uongozi wa Chuo
7. Baada ya kufanya malipo wasilisha risiti ofisi ya uhasibu ili ukatiwe na kupewa **risiti ya VETA**.
8. Wasilisha nakala ya **risiti ya VETA** katika ofisi ya Msajili ili irekodiwe na baada ya hapo **ni jukumu la mwanachuo kutunza risiti zake zote za malipo kwa muda wote wa mafunzo.**
9. Lipa fedha kiasi ulichoelekezwa tu. **Malipo yakifanyika hayarudishwi**
10. Sare na vifaa vya masomo: -
    - Vifaa vya hesabu, "Mathematical set" yenye vifaa vyake muhimu.
    - Kalamu ya mkaa/penseli zenye ubora kwa ajili ya kuchorea.
    - Daftari kubwa 8, "Counter Books", "Three" au "Four Quires", na daftari za ziada 4.
    - "Drawing pens", kalamu za wino za kuchorea – 0.25, 0.35, 0.5, 0.7, na "Set square" $45^0/60^0$ isipokuwa fani ya Uhazili na Kompyuta
    - Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta "Ream" moja ya karatasi nyeupe (A4) yenye ubora unaokubalika.
    - Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetron, yawe yanazidi sm 20 kutoka kwenye kiuno ili kuweza kuchomekea vizuri.
    - Jozi mbili ya viatu vyeusi, vya ngozi visigino vifupi na vyenye kamba.
    - Jozi moja ya viatu vya michezo
    - Sweta rangi ya bluu iliyokolea
    - Jozi moja ya viatu vya usalama kwenye karakana (safety boot), isipokuwa kwa wale wa Uhazili na Komputa wanatakiwa kuwa na viatu nyenye visigino vifupi na vyenye kamba.
    - Jozi nne (4) za soksi kwa wanawake ziwe nyeupe na kwa wanaume ziwe nyeusi.
    - Jozi moja ya soksi za michezo.
    - "Rain boots", ziwe za rangi nyeusi.
11. Vifaa vya usafi.
    - Kwa ajili ya usafi wa mazingira ya nje: kwanja, jembe lenye mpini, reki na ufagio wa "chelewa" wenye mshikio.
    - Kwa ajili ya usafi binafsi: sabuni za kufua na kuoga za kutosha, dawa za meno, ndala, ndoo ya Lita 20 moja, na ndoo ya lita 10 moja.
    - Kwa ajili usafi wa hosteli, madarasa na bwalo la chakula: ufagio laini wenye mshikio (soft broom) na ufagio mgumu wenye mshikio (hard broom), pamoja na kaushio la maji (rubber squeezer)
12. Vifaa vya chakula (watakaoishi hosteli)
    - Sahani ya chakula "material" ya mfupa au kontena yenye vyumba vyumba.
    - Bakuli ya mboga "material" ya mfupa au plastiki nzuri.
    - Kijiko cha chakula
    - Kikombe cha chai

13. Vifaa vya kulalia
    - Shuka mbili za rangi ya bluu, size 4 x 6
    - Blanketi isiyo nzito sana, ya wastani, size 4 x 6
    - Mto 1, na foronya yake, rangi ya bluu
    - Net ya mbu, pembenne, 4 x 6, nyeupe
    - **Godoro itapatikana chuoni.**
14. Maelekezo mengine
    - Mwanachuo unatakiwa kujaza fomu ya uchunguzi wa matibabu (Medical Examination Form) pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya mafunzo ya ufundi stadi.
    - Mwanachuo hatapokelewa chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu.
    - Sheria za chuo zimeambatanishwa, mwanachuo na mzazi mnatakiwa kusoma kwa makini. Taratibu zingine za chuo zitatolewa utakapofika chuoni.
    - Mwanachuo unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo.

**VET DECL FORM - IF**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**a) MWANACHUO**

Mimi ………………………………………………… nakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Namba za simu ya mwanachuo 1: ………………………… 2: ……………………………….

Saini ya mwanachuo …………………………………… tarehe ………………………………….

**b) MDHAMINI**

Mimi …………………………………ambaye ni ……………………………………………………
wa mtwaja hapo juu, nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Namba za simu ya mdhamini 1: ………………………………. 2: ……………………………….

Saini ya mdhamini ………………………………………… tarehe ……………………………….

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA WILAYA CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUNYA**

## SHERIA, TARATIBU NA MAELEKEZO KWA WANACHUO WOTE

**Ili kufanikisha mafunzo ya ufundi stadi kufanyika kwa ufanisi kila mwanachuo anatakiwa kufuata sharia,** taratibu na miongozo mbalimbali ya nchi na chuo. Kutofanya hivyo kunaweza kupelekea hatua mbalimbali za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya mwanafunzi husika. Zifiatazo ni taratibu na sheria za chuo: -

### 1. MAHUDHURIO

a) Kila mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi.
b) Mwanachuo hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote kwa sababu ya msiba, kuuguliwa au kuugua ni lazima apate kibali cha Mkuu wa chuo.
c) Mahudhurio chini ya 85% mwanachuo hataruhusiwa kufanya mtihani.
d) Ni marufuku kwa mwanachuo kuingia au kutumia simu ya mkononi sehemu yoyote inayohusiana na mafunzo ikiwa ni darasani au kwenye karakana.

### 2. MAVAZI NA USAFI WA MWILI

a) Mwanachuo unatakiwa kuvaa sare ya chuo ambayo ni suruali ya “Blue” yenye vipimo vilivyothibitishwa na chuo wakati wote unapokuwa katika mazingira ya chuo. Shati jeupe la mikono mifupi lenye nembo ya VETA lililochomekewa vizuri ndani ya suruali**. Mwanachuo atakayevaa sare ya chuo isiyokidhi vipimo atalazimika kushona/kununua nyingine.**
b) Sare ya chuo itavaliwa wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Ovaroli litavaliwa wakati wa vipindi vya mazoezi kwa vitendo.
c) Viatu vyenye visingino virefu, kandambili na viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni wakati wa mafunzo.
d) Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano hereni, pete, bangili, mkufu kwa kipindi chote cha mafunzo.
e) Mwanachuo huruhusiwi: kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, manukato yanayotoa harufu kali, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kuvaa bangili, hereni, mkufu, au urembo wowote.
f) Nywele kwa wavulana:
g) Zikatwe ziwe fupi na isiwe kipara. Hairuhusiwi kunyoa mitindo mingine na kufuga Sharubu au Ndevu.
h) Nywele kwa wasichana.
i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni). Hairuhusiwi kunyoa au kusuka mitindo nje ya iliyoruhusiwa.

**3. USAFI WA MAZINGIRA YA CHUO**.

a) Mwanachuo unatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya chuo ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo na kutokukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.
b) Mwanachuo huruhusiwi kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, wala kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
c) Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake, hairuhusiwi kupeleka meza au viti mabwenini.

**4. WIZI, UPOTEVU NA UHARIBIFU WA VIFAA**

a) Vitendo vyovyote vinavyohusisha wizi ni kosa la jinai.
b) Ukipoteza au kuharibu kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe.
c) Hairuhusiwi mwanachuo kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo bila idhini ya Mkuu wa Chuo.
d) Mwanachuo atapekuliwa au kukaguliwa wakati wa kutoka au kuingai karakana na getini.

**5. UGOMVI:** Kupiga, kupigana na kushambuliana kwa maneno ni makosa ya jinai.

**6. ULEVI:** Mwanachuo haruhusiwi kulewa au kuonekana katika sehemu za vileo, kuvuta bangi au kutumia madawa ya kulevya.

**7. MAPENZI**

a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya wanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanachuo hairuhusiwi kabisa.
b) Mwanachuo yeyote haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

**8. MIGOMO:** Kushiriki, kushawishi au kuchochea migomo ni kosa la jinai.

## JEDWALI LA MAKOSA MBALIMBALI NA ADHABU ZAKE

| KUFUKUZWA CHUO | KUSIMAMISHWA MASOMO/ KUNYANG'ANYWA NAFASI YA BWENI | KUPEWA ADHABU |
|---|---|---|
| a) Wizi, rushwa na utapeli<br>b) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji bangi.<br>c) Kupiga au kupigana<br>d) Ubakaji usagaji na ushoga chuoni<br>e) Kudharau itifaki za Taifa ikiwepo Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa VETA, n.k.<br>f) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa chuo na watu.<br>g) Kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua<br>h) Kushiriki vitendo vya ugaidi.<br>i) Utoro uliokithiri.<br>j) Kumlaza mgeni bwenini.<br>k) Kupika chakula/kutumia "heater" bwenini. | a) Kukataa adhabu halali<br>b) Kuharibu mali ya chuo<br>c) Uasherati.<br>d) Kutofanya mitihani/mazoezi bila sababu<br>e) Kufanya biashara na kujihusisha na siasa chuoni.<br>f) Kuingia na mgeni/kumkaribisha mgeni bwenini.<br>g) Kutumia vifaa visivyoruhusiwa bwenini.<br>h) Kulala nje ya chuo bila ruhusa ya Mkuu wa Chuo.<br>i) Kutumia lugha ya matusi.<br>j) Kutovaa sare ya chuo awapo nje ya chuo. | a) Kuingia maeneo yasiyoruhusiwa.<br>b) Kuingia na kifaa chochote kile kinacho fanana na vilivyoko ndani ya chuo bila ruhusa.<br>c) Kupeleka meza au viti bwenini.<br>d) Kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.<br>e) Kutotunza usafi wa mazingira ya chuo.<br>f) Kukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.<br>g) Kutozingatia usafi wa mwili.<br>h) Kutoka nje ya chuo bila ruhusa.<br>i) Kuchelewa kuripoti chuoni kabla ya 1:30 asubuhi.<br>j) Kupoteza kifaa cha chuo. |

**VET MED FORM – 1E**

## VOCATIONAL EDUCATION ANDA TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date ……………………

The Medical Officer

…………………………………………………………………

…………………………………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of trainee

…………………………………………………………………………………………………….

Please Examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an……………………………………………………………………….

Eyesight …………………………………………………………………………………………

Hearing ………………………………………………………………………………………….

Asthma ………………………………………………………………………………………….

Other serious diseases.…………………………………………………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training above.

Date ……………………           Designation ……………………………………………….

Signature and Official Stamp ………………………………………………………………….